Toleo 85 - Rajab 1445 H / Februari 2024 M

Jarida la UQAB

TOLEO MAALUM



# USHINDI KWA UJUMBE WA UISLAMU KIMATAIFA

# Ushindi kwa Ujumbe wa Uislamu Kimataifa

Mnamo Ijumaa, 19 Januari 2024, Waziri wa Usalama, Tom Tugendhat alitia saini kuwa agizo la kuipiga marufuku Hizb ut Tahrir nchini Uingereza kama shirika la kigaidi. Hiyo ni baada ya Bunge la Uingereza kuidhinisha agizo kielelezo lililowasilishwa mnamo Jumatatu, 15 Januari 2024. Agizo hili linafanya kuwa mwanachama wa Hizb ut Tahrir au kuwalingania watu kushirikiana nalo ni kosa la kiuhalifu, lililo na uwezo wa kupelekwa gerezani miaka 14, ambayo ni pamoja na kulipa faini au kuchukua sehemu ya faini. [www.gov.uk/government/news].
Sababu kuu iliyotajwa kwa kuipiga marufuku Hizb ut Tahrir nchini Uingereza ni kwamba ni kundi ambalo linachuki dhidi ya Mayahudi hususan kwa kupinga uvamizi wao wa Ardhi ya Baraka ya Palestina na kuwaua Wapalestina ndani ya Gaza!

Hakika, Uingereza kwa mara nyingine imeweka historia katika kufichua asili ya nyuso mbili za tawala za Kimagharibi za kikoloni ambazo zinadai kuwa ndio ngome za amani, walinzi wa haki za kibinadamu, uhuru wa maoni na kuandamana. Alas! Wao SIO LOLOTE bali ni pote tu la vinyago wa kisiasa wa kikoloni ambao wanatanua kwa kuvamia na kupora ardhi na rasilimali za ng'ambo huku wakimwaga damu na kuwaua watu wake. Zinazodai kuwa ni dola za kipolisi za Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Uchina zinabomoka katika maeneo yao, kwa kuwa zimefeli pakubwa kupambana na ajenda ya Kiislamu kimataifa ambayo imeshamiri duniani kote.
Maazimio yao ya mwisho ni kuzindua kwa mara ya kwanza kampeni pana ya propaganda inayolenga kuuchafua na kuutia shaka Uislamu kama mtazamo wa kimfumo pekee juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai ambao umebakia, uliojaribiwa na kufaulu. Nidhamu ya kirasilimali ya kisekula iliyoko madarakani inakaribia kuporomoka kwa kishindo ambacho hakijawahi kabla yake ikilinganishwa na kuporomoka kwa mfumo wa Kikomunisti chini ya Wasoviet. Mzunguko wa kidemokrasia wa bahati nasibu umetimia nyuzi 360 na hakuna chengine cha kudandia! Mfumo pekee ulioko ni Uislamu. Kwa kuongezea, Uislamu hautabishiki isipokuwa chini ya Serikali ya Kiislamu ya Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume.

Kwa hivyo, walinganizi wa Khilafah inayotarajiwa ndani ya Magharibi wanakabiliwa na vitisho vinavyojumuisha kubandikizwa kuwa wanachuki dhidi ya Mayahudi, wana misimamo mikali na magaidi. Fauka ya hayo, wanakabiliwa na ukatili wa kupindukia kutoka kwa tawala za kiimla ndani ya Mashariki ya Kati, Urusi, Uzbekistan, Uchina nk. Jambo la muhimu la kuzingatia ni kwamba hizi tawala za kidemokrasia zimefeli kushinda hoja kuhusu nini mbadala kwa nidhamu iliyoko na iliyofeli ya kirasilimali ya kisekula ya Kimagharibi. Hivyo basi, serikali za kidemokrasia hazina chochote cha kutoa kama mbadala isipokuwa kuwanyamazisha walinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume.

Ngamia amevunjika mgongo, matukio ya hivi karibuni yaliyoanzishwa na utawala wa Uingereza hayajatokea tu kibahati mbaya, bali ni sehemu ya kampeni ya kimataifa ya kuweka vikwazo dhidi ya kuchipuza kwa Khilafah. Wanarudia yale yale waliyoyafanya Maquraysh lakini hakuna ambalo linafanyakazi upande wao. Sera zao za ndani zinawaangamiza raia wao ambao kila siku wanaandamana wakitaka kuvifungua vitanzi vilivyokazwa shingoni mwao vya kisiasa, kijamii na kiuchumi! Kwa upande mwingine, sera zao za kigeni kama ile ya Sykes-Picot zinasambaratika na watawala wao vibaraka wa kikoloni wamejawa na wasiwasi pomoni!

Hakika, ushindi wa ajenda ya Kiislamu kimataifa unakaribia kutimia kikamilifu muda wowote kutoka sasa. Mwenyezi Mungu akitujaalia (InshaAllah). La muhimu wakati huu nyeti sio kupunguza kasi na kushughulishwa na mateke ya punda anayekata roho wa mfumo wa kirasilimali wa kisekula. Badala yake lazima tuwe makini na kupatiliza fursa na kuzidisha moto wa mabadiliko kwa nishati na ushujaa. Lazima tukumbuke kuwa sisi ni watumwa wa Mwenyezi Mungu (swt), na lazima tuyape kipaumbele maisha ya Akhera kuliko hii dunya ya muda mfupi.

Muda wote lazima iwe wazi kwetu, kwamba adui anajuwa nguvu za Khilafah yetu inayotarajiwa na hivyo anaipigia njama dhidi yake. Alas! Meli inakaribia kutia nanga bandarini muda wowote kutoka sasa. Swali msingi zaidi ni kwa gharama ipi tuko tayari kulipa kuhakikisha kuwa meli inatia nanga bandarini? Kupoteza ajira zetu, uraia, kubandikizwa tuna misimamo mikali na magaidi, kutupwa gerezani, mali zetu kutaifishwa, kuandamwa na kuuliwa kiholela miongoni mwa mengine ni baadhi ya gharama zinazotarajiwa kuzilipa. Mwenyezi Mungu (swt) alisema :
أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ ٱلَّذِينَ خَلَوْا۟ مِن قَبْلِكُمۖ مَّسَّتْهُمُ ٱلْبَأْسَآءُ
وَٱلضَّرَّآءُ وَزُلْزِلُوا۟ حَتَّىٰ يَقُولَ ٱلرَّسُولُ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مَعَهُۥ مَتَىٰ نَصْرُ ٱللَّهِۗ أَلَآ

*Endelea... UK 3*

إِنَّ نَصۡرَ ٱللَّهِ قَرِيبٌ **"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyo wajia wale walio pita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walio amini pamoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu."** [Al-Baqarah: 214]

Mtume (saw) alizungumza kuhusu zama hizi katika Hadith yake maarufu. Anas bin Malik (ra) alisimulia kwamba Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema: "يَأْتِي عَلَى النَّاسِ زَمَانٌ الصَّابِرُ فِيهِمْ عَلَى دِينِهِ كَالْقَابِضِ عَلَى الْجَمْرِ **Zitakuja zama kwa watu ambapo yule atakayekuwa na subira juu ya dini yake atakuwa kama yule anayeshikilia kaa la moto."** [Tirmidh #2260] Kwa kuongezea, Abdullah (ra) alisimulia kwamba Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema: **«إِنَّ الإِسْلاَمَ بَدَأَ غَرِيبًا وَسَيَعُودُ غَرِيبًا فَطُوبَى لِلْغُرَبَاءِ». قَالَ قِيلَ وَمَنِ الْغُرَبَاءُ قَالَ «النُّزَّاعُ مِنَ الْقَبَائِلِ» "Uislamu ulianza ukiwa kitu kigeni na utarudi kuwa mgeni, kwa hiyo bishara njema kwa wageni." Ikasemwa: 'Ni kina nani hao wageni?' Akasema: "Wageni ambao wameziwacha familia na kabila zao."** [Sunan Ibn Majah #3988] Hakika, katika zama hizi watu ambao wanakwenda mbio kurudisha tena maisha ya Kiislamu wameikataa (wametoka) nidhamu ya kirasilimali ya kisekula na inayohusiana nayo kama vile nidhamu ya kidemokrasia, sheria ya kimataifa, nidhamu ya kihuria ya kijamii – ukombozi wa wanawake!

Uingereza imepiga firimbi, wakati ni sasa wa kupambanua baina ya wachezaji wa siasa ya Kiislamu wa kweli na wanachuoni wa kisiasa. Kwa maana nyingine, hakuna njia ya mkato au mirengo miwili; ima uwe ni mchezaji wa siasa ya Kiislamu utakayepatiliza matukio ya hivi karibuni kusongeza mbele ajenda ya Mwenyezi Mungu (swt) na kuivuta rai ya ummah upande wako. Kama wachezaji wa siasa ya Kiislamu, tunatakiwa kufikiria na kutenda kwa haraka, kimahesabu na kukatikiwa. Kilichoko mbele yetu ni kuiteka rai ya ummah na sio kingine. Kilichoko cha dharura ni sarafu ya rai ya ummah ambayo yatakiwa kuchochewa kuzidi na kuelekezwa kwa suala la kiuhakika ambalo ni kuunganisha kusambaratika uhalisia wa kisiasa ndani ya Magharibi unaofichuliwa na kufeli kwa sera zake haribifu za ndani na nje zinazodhikisha dunia.

Lazima tukumbuke kwamba kufikiria kisiasa ndio kilele cha kufikiria na hivyo gharama yake ni kubwa mno lakini inayostahiki kulipwa hususan pale ambapo ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt) na sio kingine. Ummah wahitaji mashujaa ili uwape uongozi wa kisiasa, na uongozi hukabidhiwa wasioogopa, Kitendo kidogo tu cha kiujasiri wa kupindukia kitapelekea athari kubwa ambayo itayafanya Mapinduzi ya Bara Arabu ya 2011 kuwa ni mchezo tu.

Ulinganizi kwa wanajeshi Waislamu miongoni mwa majeshi ya Waislamu kunyanyuka kutoka katika kambi zao za kijeshi ndani ya Bangladesh, Pakistan, Saudi Arabia, Yemen, Egypt, Jordan, Tunisia, Uturuki nk, lazima uzidi kasi. Kila Muislamu dada, kaka, baba, shangazi au mjomba aliye na mtoto ndani ya majeshi ya Waislamu lazima aulizwe pasina kuchoka kuwalingania jamaa zao ili kutoa Nussrah (msaada wa kijeshi) kwa ajili ya kusimamisha Khilafah kupitia njia ya Utume. Hizb ut Tahrir iko tayari kwa kazi hiyo na imechapisha kielelezo cha katiba kwa upana kuonesha utayari wa kutekeleza mfumo wa Kiislamu kwa ukamilifu chini ya Khilafah iliyosimamishwa tena kwa njia ya Utume.

Kwa kutamatisha, kuibandikiza Hizb ut Tahrir nchini Uingereza kama shirika la kigaidi lazima lichukuliwe kama baraka iliyofichika na fursa ya kupatilizwa kwa ajili ya ulinganizi wa kusimamisha tena Khilafah ndani ya ulimwengu wa Waislamu. Kwa kufichua Wamagharibi katika kufeli kwao kuhimili mihemko ya Hizb ut Tahrir kama chama cha kimfumo wa Kiislamu ambacho hakitumii mabavu bali mvutano wa kifikra kama silaha yake hatari. Ili kuwavunja Wamagharibi ambao wanatizamwa na watawala wao Waislamu vibaraka wa kikoloni ndani ya ulimwengu wa Waislamu. Hivyo basi, kuzidisha ulinganizi kwa watu jumla kuelekeza maandamano yao kwa makaazi ya watawala Waislamu vibaraka ili kuwang'oa mamlakani. Kinyume chake, waelekee katika makao makuu ya kijeshi na kuwalingania Majenerali wa Jeshi kuchangamka na kuwaondosha vikaragosi wa kikoloni ambao wanaweka vikwazo katika kunyanyuka kwa mfumo mbadala wa Kiislamu. Wakati ni sasa, muda haunasi na fursa haziji mara mbili.


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro (Abu Taqiuddin)**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Sheikh Taqiuddin An-Nabhani




Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliyochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur'an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.

[وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ]

**"Na watasema: Lau kuwa tungeli sikia, au tungeli kuwa na akili, tusingeli kuwa katika watu wa Motoni!."** [Surah Al-Mulk: Aya 10]

Kupotoka kifikra kunaweza kupelekea ummah wote katika natija ya mporomoko mkubwa. Hii ndio sababu kusawazisha fikra za Ummah na kusahihisha njia yake ni moja katika misimamo mikubwa ya kishujaa. Sheikh shujaa, hakimu jasiri, mfufuaji wa fikra ya Kiislamu, Sheikh Taqiuddin An-Nabahani kijana mzuri wa Ummah huu na mwenye ari ya kunyanyuka kwake. Aliishi maisha aliyoshuhudia vurugu zilizosababishwa na kuangushwa kwa Khilafah. Alishuhudia kupenyezwa kwa thaqafa ya Kimagharibi na kusambaratishwa kwa mawazo na mashirika tofauti ya ufisadi dhidi ya fikra safi ya Uislamu katika mabongo ya watu, kama Uzalendo, Utaifa , Ufrimasoni, Umaksi na nyinginezo. Na nyuma ya hii mifumo kulikuweko na maelfu ya makhaini. Alishtushwa na Nakba ndani ya Palestina, ambaye ni kijana wake. Akaisoma michakato mingi tofauti ya Kiislamu kwa ajili ya kuleta mabadiliko. Angelikata tamaa na kujitenga na watu au akachukua uamuzi wa kujifunga na Dawah ya kivitendo ya kibinafsi kama walivyofanya wengine. Hata hivyo, yeye (rahimahuAllah) alichukua msimamo wa kishujaa wa kifikra ambao unachukuliwa tu na watu wakubwa wenye fikra na waliokata shauri.

Sheikh alihifadhi Qur'an akiwa na umri wa miaka 13 kisha akasoma Kiarabu na sheria, na akafikia kiwango cha juu cha Kishari'ah ndani ya Chuo Kikuu cha Al-Azhar. Aliyasoma kwa kina mashirika na harakati zilizokuwepo wakati wake na kuweza kutambua makosa ambayo wengi walikuwa nayo; udhaifu wa fikra ya Kiislamu na kutiwa sumu kwake na uchafu wa Kimagharibi ambao umevamia ardhi. Sheikh alianza kukutana na mashirika tofauti ya Kiislamu na uongozi wao wakati alipokuwa Al-Azhar nchini Misri vilevile ndani ya Palestina alipokuwa hakimu katika Mahakama ya Al-Quds, alijadiliana nao na kuwasilisha kwao mawazo aliyokuwa nayo. Wakati huo huo , alikuwa akifanya mijadala na waliobeba fikra za kisekula (masekula),

*Endelea... UK 5*

kitaifa, kijamii na mifano yao. Alijumuisha ukali katika kushambulia fikra zisizokuwa za Kiislamu, na kwa heshima na upole alipokuwa akijadiliana na vyama vya Kiislamu licha ya tofauti zao kwa kuwa sehemu ya njia ya Nabhani ilikuwa ni kujiepusha kutokamana na kushambulia watu na mashirika ambayo yanafanyakazi ya Uislamu. Pia alikuwa na sifa ya kuwa mkarimu kwa Ummah wake na kutouhesabu kwa kuporomoka kwake kama wanavyofanya wengine kwa masikitiko. Alikuwa anameremeta kwa maarifa, nishati na ufikiriaji wa kina, uwezo wa juu wa kukinaisha wengine, hakuwahi kupumzika, alikuwa mchangamfu kwa sababu ya vidonda vya Ummah wake.

Baada ya usomi wa kina na sahihi, Mwenyezi Mungu (swt) alimpa ushindi Sheikh Taqiuddin katika kutambua chanzo cha maradhi ya Ummah ambacho ni kutokuwepo kwa dola ambayo inatekeleza nidhamu ya Uislamu, hivyo kuwasimamia watu na kuwakinga na maadui zao. Pia alielekezwa kwa njia ya Utume katika kuunyanyua Ummah na kurudisha tena maisha ya Kiislamu: kuanzisha chama miongoni mwa vijana wa Ummah, ambacho kinauchukua Uislamu kuwa ni mfumo wa kisiasa, kinachotaka kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena Khilafah Rashidah iliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu (swt) na Nabii (saw). Sheikh alianza kutoa Khutbah na mihadhara ndani ya msikiti Al-Aqsa, ndani ya Al-Khaleel na miji mingine ndani ya Palestina, akiwaonyesha Waislamu uwajibu wao na kushambulia tawala za Kiarabu kwa kusema zimebuniwa na Wamagharibi Wakoloni. Alikuwa akifichua mipango ya kisiasa ya dola za Kimagharibi na nia zao dhidi ya Uislamu na Waislamu. Alikutana na Wanachuoni aliokuwa akiwajua na kuwapa fursa wajiunge naye katika kazi yake mpaka akafaulu kuwakinaisha kikundi cha Wanachuoni na Mahakimu watajika na kujitunukia harakati zake kwa kubuni Hizb ut Tahrir mnamo mwaka 1952 licha wote wao kutambua hatari ya walichokuwa wanakaribia kuanza.

Hizb ilianza Dawah ndani ya Al-Quds na maeneo pembezoni mwake. Walio na madaraka walitambua hatari ya Dawah hii kwa hiyo kwa haraka wakaanza kuishambulia Hizb, kuipiga marufuku, kufunga afisi zake na kuwashika wanachama wake. Mamlaka ya Jordan na Palestina wakaitia korokoroni Hizb. Hata hivyo, Alhamdulillah, hili likasadifiana na kuenea kwa mawazo ya Khilafah nchini kote. Haswa, nuru yake iling'aza nje ya mipaka. Sheikh hakulingania Khilafah kama mwito tu. Bali alifaulu kuzalisha kwa upana mipangilio ya Kishari'ah kabla ya na baada ya kusimamishwa Khilafah. Akaipangilia njia ya Kishari'ah ya Mtume ya kusimamisha Dola ya Khilafah. Pia akafafanua muundo wa Dawah wa kidharura kwa ajili ya kupangilia safari ya Chama kufanyakazi ili kusimamisha Dola hii katika njia ambayo itailinda kutokamana na kupotoka na kuganda. Yeye (rahimahuAllah) akazalisha kwa kina maalumat ya kina ya Kiijtihadi kuhusiana na nidhamu zote ndani ya Dola ya Khilafah katika utawala, uchumi na nyinginezo.

Kisha awasilisha kwa Ummah, maalumat makuu ya kifikra ambayo hayajawahi kufanywa na yeyote kabla yake: katiba kamili ya Dola ya Khilafah iliyochipuza kutoka ndani ya nuru ya Qur'an na Sunnah, ikijumuisha taasisi zote na vitengo vyake vyote, tayari kwa ajili ya utekelezwaji punde tu ikisimama! Sheikh alishikwa mara nyingi na kuteswa. Alihamia Damascus, akapanda matunda mazuri ya Dawah yake huko na kuonja ukali wa magereza yake na viboko vyake. Mawimbi ya makatili yakamsukuma nje na kwenda Iraq na kisha Lebanon ambako mateso yalimzidi na roho yake kumtoka na kurudi kwa Muumba wake. Akiwacha nyuma chama cha kisiasa cha kimataifa ambacho kimechipuza kutoka katika Ardhi ya Baraka na kufikia zaidi ya nchi 50 na Khilafah hivi sasa ni mwangwi ambao unakera na kutishia vitanda [vya makatili], unaoonekana na kusikika kila mahali. Wanachama wake wanafanyakazi mchana na usiku, wakizuia mashambulizi ya Wamagharibi na kuunyanyua Ummah wao ambao unawakumbatia kila kukicha, na Masekula na wanaopigia debe ufisadi na upotoshaji wanawakimbia. Mwenyezi Mungu amrehemu Taqiuddin An-Nabhani na aturuhusu tushuhudie kufaulu kwa lile ambalo aliutumia uhai wake ambalo ni kuona: Khilafa Rashidah inayoeneza nuru ya haki duniani kote baada ya kuzama ndani ya dhuluma na ukandamizaji.

# Sayyid Qutb



Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliyochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur'an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.


Tofauti baina ya njia sahihi na njia ya salama ni kama tofauti baina ya ushujaa na kutokomaa. Hii ni hususan pale ambapo njia sahihi sio maarufu katika kipindi cha makubaliano. Shahidi shujaa, Sayyid Qutb aliishi katika zama ambapo zilifuatia kuvunjwa kwa Dola ya Kiislamu. Majeruhi ya hadhara ya Kimagharibi, na kupenya kwa Usekula baina ya Waislamu; lakini tukio lililomshitua zaidi na kumchochea ni kuchipuza kwa mapendekezo yanayodai kuwa ni ya Kiislamu na kujaribu kiuhadaifu kuchanganya Uislamu na hadhara nyingine. Mapendekezo yaliyoihama Dawah ya kuifanya Shari'ah ya Mwenyezi Mungu (swt) kutawala, na kuchukua misimamo duni iliyolingania kushirikiana na madhalimu na kujumuika katika nidhamu za Kijahiliya kwa ajili ya usalama na kupata manufaa. Sayyid alichukua msimamo wa kishujaa na wenye maono ya kina. Kupitia kwayo, alikataa hali iliyokuwepo ya kulazimishiwa na Wakoloni. Alidai watu watawaliwe na Uislamu kwa ukamilifu na kurudishwe Khilafah iliyokuwa imedondoka. Alikabiliana na ufisadi wa mamlaka na hakukubali mapendekezo yao ili kununua hotuba zake au kumnyamazisha. Alisema: "Dhalimu kiuhalisia si chochote bali ni mwanamume asiyekuwa na nguvu wala madaraka. Bali ni ummah ambao haujitambui na umejisalimisha na kupeana migongo yao ili kukaa juu yao, kuzipeana shingo zao ili alizuburuze, unashusha vichwa vyao ili kuwa bwana juu yao kusalimisha haki yake ya kuwa na hadhi kwake ili aivunje." Aliwakabili watu wa njia ya usalama na Mafaqih wa makubaliano. Aliingia katika mijadala nao, na kuzivunjilia mbali fahamu zao za kimakosa, na kuthibitisha kwamba mageuzi ya kweli yanaweza kuwa kwa njia ya kimsingi pekee, na wala kazi za kutiaviraka sio kazi ya mitume bali ni kuwafanyiakazi madhalimu na kuendeleza uwepo wake.

Katika aliyoyasema ni: "Ikiwa umetumbukia katika matope ya makubaliano basi usiwapige vita walio imara na kusema kuwa wana misimamo mikali. Badala yake, angalia mguu wako ili utambue kuwa umekwama katika matope." Haiwezikani kwa Uislamu kukubali au kukubaliana kuwa ni sehemu ya Uislamu na sehemu ya Ujahiliya. Matokeo yake kama yalivyo tarajiwa ni kwamba Sayyid alitiwa gerezani na mamlaka ya kidhalimu kumkandamiza kama ilivyo kwa kila ambaye aliifuata njia ya mitume. Hata hivyo, yeyote anayefikiria kwamba kumtia mtu gerezani ni kunyamazisha ukweli atavunjika moyo. Kwa Sayyid alipatiliza miaka yake ya gerezani kuwapa Ummah moja katika Tafsiri adhimu za Kitabu cha Mwenyezi Mungu (swt): "Katika Kivuli cha Qur'an." Hakuzungumzia kuhusu mateso ya gerezani. Alizama ndani ya maana ya maneno ya Mwenyezi Mungu (swt) na kuyatabikisha juu ya uhalisia fisadi ambao Ummah wake ukiishi ndani yake. Aliiwasilisha kama mshono katika vidonda vya Ummah na dawa kwa mateso yake. Sayyid alikuwa anausukuma Ummah wake kuleta mabadiliko na kujaribu kuuamsha kutoka usingizini. Alikuwa akisema: "Udhalimu hauogopi chochote kama ilivyo kwa watu walio makini wenye

*Endelea... UK 7*

utambuzi na mioyo iliyo jaa tahadhari, na haumchukii yeyote kama unavyomchukia yeyote anayelingania utambuzi na utahadhari, na hauna kinyongo dhidi ya yeyote kama ulivyo na kinyongo zaidi kwa wale wanaoamsha akili zilizo lala.” Alielezea kwa kina fahamu kuhusu Hekimiya (Ubwana) na kwamba hiyo ni haki pekee ya Mwenyezi Mungu (swt), hakuna ambaye ana nafasi katika hilo Naye. Alimakinisha kwamba ni wajibu kiukamilifu kutofautisha ukweli na urongo. Sayyid alifungwa gerezani lakini kivuli chake kiliangaza kutoka huko na kusafiri kila pembe na kuwaamsha waliokuwa wamepotea na kuwafufua waliokufa na wasiotambua. Mwenyezi Mungu (swt) alikuwa amejaalia iweze kukubaliwa na wengi na kusambaa. Makatili waliona ni jambo la dharura kumuua mara moja kwa kuwa amekuwa mwanamume tishio la uhakika kwa hali iliyopo ambayo haikuweza kuhimili kukabiliana na uimara wake. Sayyid aliuliwa lakini maneno yake yenye kuangaza na misimamo yake mikubwa haikufa. Alikufa akiwa na hadhi. Jina lake linaendelea kuishi ilhali majina ya maadui na waliompinga yamefifia. Walimpa fursa ya kuchagua kama walivyompa Al-'Izz bin Abdussalam, kama wakuu kabla yake: “Utarudi nyuma na kumuunga mkono mtawala?” Alijibu: “Kidole cha shahada ambacho kinashuhudia upweke wa Mwenyezi Mungu (swt) kinakataa moja kwa moja kuandika hata herufi moja katika kuunga mkono utawala wa kidhalimu.” Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu Mwanachuoni mchamungu, mwanasiasa mkomavu na mwanafikra wa kimfumo, Sayyid Qutb aliyefariki akiwa huru nyuma ya kuta hizo, aliyefariki akiwa huru ndani ya minyororo hiyo. Kinyume na vifo vya waliosalimu amri na wale walio lazimisha kuoanisha Uislamu na Ukafiri historia imeyafuta majina yao na hawakupata radhi za Bwana wao wala za adui wao ambaye walimkasirisha Bwana wao. Badala yake, adui wao aliwatema nje kama koozi punde alipokuwa hawahitaji tena. Ujumbe kwa mashirika ya Dawah leo: Jifunzeni kwamba Uislamu ni wakipekee na kattu haukubali kugawanywa wala kupunguzwa. Na hauna mambo mengi kwa mujibu wa kipimo cha madhalimu. Kwa hiyvo, yeyote atakaye uchukuwa kama ulivyo basi lazima auchukue, kisha atakuwa anajipa uhai mwenyewe na Ummah wake. Ewe Mwenyezi Mungu (swt) hakuna utawala wa haki isipokuwa Wako kwa hiyo tufanye tuishi kama walinzi wake au tupe kifo kama mashahidi tukiwa twajaribu.

# Sheikh ul Islam Ibn Taymiyyah...
# Mwanachuoni wa Kisiasa Mpiganaji



Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliyochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur'an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.

Mwanachuoni anapochanganya Fiqh ya kina, nguvu katika kutoa hoja na ujasiri katika muhasaba na ukali katika Jihad, basi huo ni ushujaa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt). Umesawiana umri wa Sheikh ul-Islam Ibn Taymiyya alioishi na zama zetu leo. Alishuhudia makruseda wakivamia ardhi na kushuhudia vibaraka wakiwafanyiakazi wavamizi. Aliishi zama zama vita baina ya Waislamu. Sheikh ul-Islam Ibn Taymiyya aliishi ndani ya vita hatari zaidi vya aina yake dhidi ya Ummah. Kwani katika zama zake wasioamini mungu, wanafilosofia na waliokengeuka walikuwa wamezidi. Hata hivyo, haya yalisadifiana na mporomoka wa Ijtihad – bali kukatika kwa Ijtihad. Taqleed ikawa imeenea na ufikiriaji wa Kimadhab ulikuwa umekita katika suala la Fatwa. Na kuenea kwa ushabiki na muono mfupi kuhusiana na mambo na hatari mpya. Kwa kuongezea, utawala ulikuwa hauna uchamungu na ulikuwa ni wa kikatili na ukandamizaji.

Katika kukabiliana na uhalisia huu muovu, Mwanachuoni Ibn Taymiyya hakuamua kuuacha Ummah wake uliojeruhika na kujitenga na watu kwa kutumia udhuru wa kuepuka Fitna na kujirekebisha binafsi. Hakuamua kuwaacha watawala makhaini kwa kutumia udhuru wa kutii Wali ul-Amr kama wanaowaabudu watawala leo. Bali, aliamua kuasi hali yote iliyokuwepo. Maisha yake yamejaa misimamo ya kishujaa. Alizama ndani ya elimu (maarifa ya Kiislamu) na kunywa kutoka kwake kwa kina. Kisha akaanza kuchapisha na kufunza mapema, na kufufua elimu. Akaelezea kwa kina Hukm za Kishari'ah juu ya masuala mapya zama zake. Alikuwa akienda jangwani kuandika na lau atakwama kuhusiana na jambo fulani, ataswali , akiuweka uso wake mchangani na kuomba Du'a kwa Mwenyezi Mungu: "Ewe Mwenyezi Mungu, Mwalimu wa Ibrahim, nifunze. Mfafanuzi wa Sulayman, nifafanulie."

Alikuwa akiwajibu wasomi wa Kalam na wanafilosofia na kufanya mijadala nao kifikra. Pia akasitisha kupotosha na kuzua kwingi ambako kulikuwa kumeenea zama

*Endelea... UK 9*

zake ilhali Wanachuoni walikuwa hawamnazo. Kisha akaelekeza umakinifu wake kwa wavamizi. Kwa hiyo, akaandika kuhusu siasa ya Kishari'ah, Jihad na majukumu ya mtawala na dola. Machapisho yake yamekuwa ni marudio ya kifikra na Fiqh hadi leo. Akaungana na Ummah wake katika Jihad dhidi ya wavamizi. Alisafiri kwenda Cairo ili kumlingania Mamluk Sultan kutumana jeshi kwenda Ash-Shaam. Watu wa Ash-Shaam wenyewe walimteua yeye akazungumze na Tartar Sultan kwa niaba yao. Kwa hiyo, kwa ujasiri alikutana naye na kumfanya asikize yale ambayo viongozi na makamanda hawakujaribu kumwambia, alimwambia: "Babako na Babu yako walikuwa Makafiri na wewe leo wadai kuwa ni Muislamu, ilhali wao walikuwa waaminifu zaidi kwa mikataba yao."

Pia akautia motisha Ummah kupigana Jihad. Alitoa Fatwa kuhusu uwajibu wa kumfurusha mvamizi. Aliwahamasisha Waislamu wa As-Shaam, Misri pamoja na Waarabu Mabedui kupigana. Alishiriki Jihad akiwa nao mpaka pale Mwenyezi Mungu (swt) alipowapa ushindi na Matartar wakasambaratika. Sheikh ul-Islam alikuwa hana usalama kutokamana na maadui zake. Maadui zake walipiga njama dhidi yake na kupata uungwaji mkono kutoka kwa baadhi ya Masultan, kwa hiyo alitiwa gerezani mara 7 ndani ya Ash-Shaam na Misri. Alikuwa akitumia muda wake gerezani kwa kuandika na kufunza. Alipokuwa gerezani, alimuandikia barua mtawala kuhusu kurekebisha hali za magereza na majukumu ya dola.

Ilijumuisha uhitaji wa kuwafunza walioko gereza. Mshangao ni kwamba mtawala alitekeleza mapendekezo ya Ibn Taymiyyah. Mlima wa maarifa, Ibn Taymiyyah, alifariki gerezani miongoni mwa wanafunzi wake kama Ibn Al-Qayyim na Al-Ghayyani na wengine. Miongoni mwa lulu aliyoisema na kusambazwa kwa vizazi: "Maadui zangu watanifanya nini? Bustani na pepo yangu iko kifuani mwangu, kuniua ni Shahadah, kunifunga ni Khulwa (na Mwenyezi Mungu (swt), na kunitoa mjini ni kutembea." Mwenyezi Mungu amrehemu.

Sheikh ul-Islam aliondoka, akiwacha nyuma thurati kubwa ya zaidi ya vitabu 500 na maelfu ya barua na Fatwa. Alishiriki Jihad kwa uhai wake, mali na kalamu na alikataa kusalimu amri kwa madhalimu au kunyamaza kimya juu ya upotoshaji wala kukubali hongo katika Dini. Kaka na dada, ulingo wa Dawah uko wazi leo kwa walioamua. Silaha kubwa aliyokuwa nayo Sheikh ul-Islam ilikuwa ni elimu na fikra ya Kiislamu, kupitia kwayo alikiangamiza kiza cha ujahiliya na kuzifurusha takataka za wanaozusha – na ni wangapi hii leo. Twajifunza kutoka kwake dori ya ujasiri wa Mwanachuoni ambaye amejifunga na yale yanayowahusu watu na ndio chungio inayochuja vitisho katika kufikiria kwao na chochote ambacho kitaharibu fahamu zao. Twajifunza kuhusu dori ya kisiasa ya Mwanachuoni anayewahesabu watawala na kuyakashifu maovu yao. Kwa masikitiko, idadi kubwa ya Wanachuoni leo wamesalimu amri na kuuwacha Ummah kutekwa na mawimbi ya Fitna. Leo, twaishi katika zama za fahamu za mkanganyiko, kutikiswa kwa misingi na kushambuliwa kwa matukufu. Kwa hiyo, wako wapi walio imara ambao watailinda Dini yao, kuwahesabu wakandamizaji, kuuamsha Ummah wao na kuleta mabadiliko yatakayoupelekea Ummah katika Khair na wasioogopa kuhusiana na yatakayowapata kwa ajili Yako.

# Abdullah bin Umm Maktum – Ushujaa wa Kuupiku Ulemavu

Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliyochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur'an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.

Kuna misimamo ambayo imetikisa mbingu na malaika kushuka, na Mitume wameizungumzia. Abdullah bin Umm Maktum (ra) mwanamume kipofu aliyeshindana na wanaoona, na kuwashinda baadhi kwa umbali mno. Yeye (ra) angelitumia ulemavu wake kama udhuru na kuwawachia uwanja wengine na kuishi kama wengine miongoni mwao. Hata hivyo, yeye (ra) aliuchukuwa Uislamu alioujuwa kama mfumo na ambao aliutumikia kwa uhai wake na juhudi zake kwa kadri ya uwezo aliokuwa nao.

Yeye (ra) alikuwa mmoja katika Waislamu wa kwanza kuingia katika Uislamu. Ibn Umm Maktum (ra) aliondoka nyumbani kwake, akiwa kipofu, na kuharakisha akitaka kujiunga na darasa la Nabii (saw). Darasa hatari ambalo kwamba Maquraysh wanawasaka madhaifu wake kama yeye wanaohudhuria ili kuwaadhibu na kuwatesa. Licha ya yote hayo, kipofu huyu haingii wasiwasi au kujali kuhusu matatizo wala kusitasita. Yeye (ra) bali alihudhuria darasa. Hata hivyo, Nabii (saw) alikuwa anazungumza na kundi la viongozi na watajika miongoni mwa Maquraysh na alikuwa anawalingania kwa ukakamavu waingie katika Uislamu japo angalau mmoja wao aingie katika Uislamu na ipelekee kupungua kwa mihemko kwa Waislamu. Kipofu akaja: "Yuko wapi Nabii (saw)?" "Ameshikika na kuwalingania Makafiri Maquraysh." Ingelimtosha Abdullah (ra) kukaa na kusubiri mwalimu kumaliza shughuli zake. Lakini kiu chake cha kupata elimu kikamfanya asiweze kusubiri. Akamuendea huku anatapatapa na kumtafuta mpaka akamfikia Nabii (saw) na kumuingilia kati na kumvuta upande wake: "Nifunze, Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu" "Niongoze, Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu." Nabii (saw) akamtizama pasina kusema hata neno moja. Akakunja uso kutokamana na kumuingilia kati kama ambaye anamwambia: "Ewe Abdullah, nisubiri kidogo. Hunioni nimeshika na hawa watu wenye nguvu ambao natafuta msaada wao kwa ajili ya Dini?" Sasa fikiria! Kaka na dada, kipofu hakuona mkunjo wa uso na licha ya hivyo, malaika wako katika ugomvi na hivyo wahyi ukamshukia Nabii (saw) wetu: عَبَسَ وَتَوَلَّىٰٓ* أَن جَآءَهُ ٱلْأَعْمَىٰ **"Alikunja kipaji na akageuka! Kwa sababu alimjia kipofu!"** [Abasa: 1 – 2].

Wahyi umekuja kuunga mkono msimamo wa Abdullah, kumuhesabu bwana wa viumbe na kuwaweka watu makundi baina ya "Lakini kwa yule aliyekuja kwako kwa juhudi akitafuta [elimu]" na baina وَأَمَّا مَن جَآءَكَ يَسْعَىٰ **"Ama anaye kujia kwa juhudi."** [Surah Abasa: Aya 8] Na Quran imemuamrisha Nabii (saw) Wake kuwaelekea kwa ukamilifu wale ambao wamewajia kwa juhudi wakitaka Uislamu hata kama ni madhaifu na wasiojiweza. Na wala asiwape kipaumbele wenye nguvu ambao wanauepuka Uislamu. Kwani ushindi hautakuja katika mikono ya wenye kujipiga kifua. Lakini usihofu Ewe Muhammad kwa kuwa hii Dini tukufu Inabebwa kwa mikono ya malaika wajumbe, watukufu na watiifu." Ni somo la kina lililoje kwa Nabii (saw) wetu na kwetu, Ummah baada yake. Dini yetu tukufu inafuata wala haifuati. Wanaoitaka watakuja, wataifuata na kubadilika kupitia kwayo na wala haiwafuati wao. Aya kumi na sita zimetoa masomo kuhusu hadhi na utukufu. Kipofu alikuja darasani kuja kusoma lakini aligeuka na kuwa mwalimu. Kiasi kwamba Nabii (saw) alipomuona alikuwa akisema: "Mkaribisheni yule ambaye Bwana wangu alinihesabu." Surah 'Abasa pia ikiitwa Surah Al-A'ma (mwanamume kipofu) sio kwa maana ya sifa ya ulemavu bali kwa kumtunukia mwanamume kipofu aliyeupiku ulemavu na kuwa ndio sifa ya kumpandisha daraja. Misimamo ya kishujaa ya Adullah bin Umm Maktum (ra) haikubakia tu katika tukio hilo. Bali maisha yake yalikuwa yamejaa mfano kama hiyo. Na Ayah ""**Ama anaye kujia kwa juhudi.**" ilimfuata maishani mwake. Kwa kuwa aliwashinda wengine na kuondoka mjini mwake na kuhamia Madinah. Alimpata Mus'ab (ra) akiwalingania watu kwa hiyo akamsaidia na kuisoma Quran, kuwafunza Ansar. Kwa kuwa alikuwa miongoni mwa Masahabah (ra) aliyekuwa amehifadhi kiasi kikubwa cha Quran. Alipata utamu katika sauti yake na hivyo wakashirikiana na Bilal bin Rabah (ra) katika kuadhini. Nabii (saw) alimuona ni muweza katika kutawala. Hebu fikiria! Nabii (saw) alimpa unaibu wake kusimamia Madinah mara 13! Hata mwito wa Jihad ulipopigwa, kipofu alikuja kwa juhudi ilhali akimuogopa Mwenyezi Mungu (swt), akiwacha nyuma udhuru wote. "Ewe Abdullah, utafanya nini katika jeshi miongoni mwetu? Alikuwa akiwajibu: "Nitasimama baina ya mistari

*Endelea... UK 11*

na munipe bendera ni wabebee.” Na yeye (ra) aliendelea kuwa na juhudi mpaka alipopata shahada katika Qadisiya akibeba bendera ya Uislamu.

Kaka na dada mulio na uwezo, ni mara ngapi leo tunasikia udhuru huu na ule ili mtu awache Dawah au kuzembea ndani yake” Mwanamume kipofu ameshiriki katika kupata elimu, Dawah, Kuadhini, Kutawala na Jihad. Na pia akatufunza kwamba wabebaji wa Dawah na wanafunzi wa elimu wako chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu (swt) na wana msaada Wake. Na pia akatufunza kwamba tusiwafadhilishe wenye nguvu kwa kutaka msaada wao. Kwa hiyo, nyanyukeni na mubebe bendera ambayo ilibebwa na mwanamume kipofu na kuwatikisa madhaifu. Na tusiwe miongoni mwa wale ambao wanajiweka mbali kisha Mwenyezi Mungu ajitenge nasi.



# As’ad ibn Zurara – Ansari wa Kwanza

Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliyochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur’an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.

Unapopata kuwa ukweli umekataliwa na kila mtu kutokana na hatari yake na kujiweka mbali nao kutokana na kuwa sio jambo la kawaida, basi unajipiku na kujipa changamoto, na kupiga hatua pale ambapo wenzako wamesalimu amri na huo ndio ushujaa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt). Nabii (saw) alikuwa anajiwasilisha mbele ya watu kwa miaka kumi. Mamia ya watu walisikia Dawah yake (saw). Zaidi ya dola (makabila) 20 walisikia kile ambacho anakilenga yeye (saw). Mwanamume ambaye amekanwa katika eneo lote kutokana na hatari ambayo Yeye (saw) alikuwa nayo, na Waarabu walimuonya kila mtu kutozungumza naye (saw) or kutomkaribia yeye (saw). Katika muktadha huu, As'ad bin Zurara (ra) anakuja Makkah miongoni mwa watu 6 – Khazraj. Kwa ghafla, mwanamume hatari anawaingilia. “Nyinyi ni watu gani?” “Ni kundi kutoka kwa Khazraj?” “Kutoka kwa washirika wa Mayahudi?” “Naam. “Je, mwaweza kukaa nikawazungumzia?” Wakasema sawa. Wakakaa naye (saw). Yeye (saw) akawalingania Uislamu kwa kuwasomea Quran. As’ad akasimama na kuwaambia watu wake. Huyu ndiye, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt), Mtume (saw) ambaye Mayahudi wamekuwa wakitutishia kumuhusu. Musimuache wampate Yeye kwanza. “Akimaanisha, “kubalini.” Wakubali na waachane na mwenendo wao wa maisha wa mababu zao, ushirikiano wao na Mayahudi, watupilie mbali propaganda za vyombo vya habari ambazo zinawatia hofu na wajiandae kwa hatari itakayowakabili kutokana na msimamo huo. Ni ushindi gani juu ya nafsi na utambuzi ulioje na ushujaa ambao Mwenyezi Mungu (swt) aliompa kijana huyo mdogo aliyekuwa mwanzoni mwa miaka ya ishirini? Yeye (ra) alikuwa ndiye Muislamu wa kwanza kutoka kwa Ansar na, ujumbe huo hakika ulikuwa Waislamu kupitia mikono ya Mtume (saw), na kuleta furaha katika macho Yake matukufu kwa mara ya kwanza baada ya kufeli mara kadhaa katika jaribio lake na kukatiliwa kidhalimu. Kisha, As’ad (ra) akamwambia Nabii (saw): “Tumewawacha nyuma watu wetu (huko Yathrib) na hakuna watu wenye uadui na chuki baina yao kama wao, lakini lau Mwenyezi Mungu (swt) atawaunganisha chini yako basi utakuwa mtu mwenye nguvu kweli.” Ulijuaje kuwa As’ad (ra), kwamba Dawah ambayo ameisikia tu hivi sasa msingi wake - La ilaha illa Allah – alijuaje kuwa Dawah hii ina uwezo wa kuunganisha mahasimu wakubwa na kusitisha umwagikaji wa damu baina ya Aws na Khazraj? Ni utambuzi gani wa kisiasa ambao shujaa huyu alikuwa nao kuhusiana na Dawah ya Kiislamu!

Kisha As’ad (ra) akarudi na kuchukua jukumu la kueneza Uislamu miongoni mwa watu wake, Khazraj ndani ya Madinah. Haswa, baadhi ya Aws – maadui – waliingia katika Uislamu pamoja naye na akarudi mwaka mwingine akiwa miongoni mwa wanaume 12 ili kumpa Bay’ah ya kwanza Nabii (saw) kisha wakarudi Madinah lakini mara hii wakiwa na balozi wa Uislamu, Musab bin Umayr (ra). As’ad (ra) alikuwa ni mshauri wa Musab na kubuni kituo ambacho MusaB (ra) alishukia hapo.

Kulikuwepo na Dar ul-Arqam ndani ya Makkah na Dar ul-As’ad bin Zurara ndani ya Madinah. As’ad alikuwa akiwakusanya watu kwake na kumuwasilisha kwa viongozi wa makabila pasina kujali hatari iliyomkabili. Alikuwa na Musab (ra) katika mizunguko yake yote. Yeye ndiye aliyemuwasilisha Musab (ra) kwa viongozi wa Aws: Sa’d bin Mu’adh na Usayd bin Hudhayr. Na akamshauri kwa kusema: “Huyu ndiye kiongozi wa watu wake, kwa hiyo kuwa mkweli kwa Mwenyezi Mungu kumuhusu.” Yeye (ra) pia alikuwa ni katika nyota wa Bay’ah ya pili ya Aqaba – Bay’ah ya Vita – muhimu mno. Haswa, alikuwa na umri mdogo kabisa miongoni mwa wanaume 70 waliotoa Bay’ah, na Nabii alikuwa amemchagua kuwa muwakilishi wa watu wake. Katika Aqaba, alikuwa ameushika mkono wa Nabii na kuwalingania wawakilishi, akisema: “Enyi watu, mwajuwa munachokitolea ahadi ya utiifu kwa Muhammad (saw)? Munatoa ahadi ya utiifu Kwake kupigana na Waarabu na wasiokuwa Waarabu, watu na majinn!”

Kaka na dada, mutaamini vipi kuhusu hii misimamo ya kishujaa iliyofanywa na mwanamume ambaye alikuwa bado hajafika miaka 25? Utaamini kwamba umri wa As’ad (ra) ndani ya Uislamu ulikuwa miaka 3 pekee? Alifariki tu baada ya Hijra na hakushiriki Badr wala Uhud, wala Jihad au ukombozi wowote? Lakini, utukufu wa misimamo yake imeghubikwa na ushujaa. Ewe kijana! Naam, waweza kufanya yaliyofanywa na As’ad (ra). Naam, waweza kutoa ahadi ya utiifu kwa mradi wa kusimamisha Dola ya Khilafah. Waweza kukataa “machafuko” yanayobuniwa kwa ajili yako na watawala ili kukutia hofu na kukuweka mbali na Dawah ya kisiasa ya Kiislamu. Mwaweza kuwalingania familia zenu na watu wenu, na kuwawasilisha kwa Du’aat, na kufungua miji yenu kupokea Dawah. Mwaweza kuupamba ujana wenu kwa kueneza na kunusuru Dawah hii, ili misimamo yenu ifunzwe ndani ya Vyuo Vikuu vya Dola ya Khilafah siku zijazo kama tunavyoifunza misimamo ya As’ad bin Zurara (ra) leo. Hivyo basi, nyanyukeni mufanyekazi ili sote tuweze kushuhudia yale ambayo As’ad bin Zurara (ra) alitaka kuyaona: “Ushindi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) na ukombozi wa karibuni.”